BASELINE EXAM

KISWAHILI

FULL NAME_____ **SCHOOL** _____

Chagua jibu mwafaka ili kujaza nafasi 1-15 zilizoachwa wazi.

Safari _1_ ilikuwa _2_ sana _3_ ilituchukuwa karibu _4_ wa _5_ manane. Wakati _6_ Limuru, wanafunzi wengi walikuwa wamechoka vilivyo. Tulisimama hapo kupunga hewa kwa wakati _7_ kisha tukaingia tena _8_ basi _9_ na kung'oa _10_.

	A	B	C	D
1.	letu	wetu	yetu	zetu
2.	ndefu	refu	mrefu	mirefu
3.	naye	nalo	nao	nayo
4.	muda	miadi	siku	masafa
5.	masaa	masiku	saa	dakika
6.	walipofika	tulipofika	tukifika	tulivyofika
7.	mchache	mfupi	fupi	chache
8.	katika	kwa	na	kuwa
9.	yetu	wetu	chetu	letu
10.	mwendo	tanga	nanga	safari

Ala za matamshi ni vile _11_ vya mwili wa mwanadamu vinavyohusika kwa njia moja au vingine na utamkaji. Mtu _12_ hutumia viungo fulani. Viungo hivyo _13_ na uzungumzaji kwa viwango anuai. _14_ huhusika sana, vingine _15_, huku vingine navyo vikitumika kidogo tu.

	A	B	C	D
11.	vungo	viungo	vifungo	vifunguo
12.	akizungumza	atazungumza	azungumzapo	azungukapo
13.	uhusishwi	huhusika	uhusiki	huhusishwa
14.	mengi	wengi	Baadhi	kidogo
15.	sana	kadiri	kidogo	kadori

Chagua jibu lililo sahihi ili kujibu swali la 16 hadi 30.

16. Wanapoishi -_____ ni safi.
- **A) nako**
- **B) nao**
- **C) namo**
- **D) napo**

17. Alimwibia naye akamwibia, kwa hivyo.
- **A) Waliibana**
- **B) Waliibania**
- **C) Waliibiana**
- **D) Waliibanga**

18. Andika umoja wa sentensi hii.
Kuta zingine zimejengwa.
- **A) Ukuta mwingine umejengwa.**
- **B) Ukuta nyingine umejengwa.**
- **C) Ukuta mwingine zimejengwa.**
- **D) Ukuta mwingine imejengwa.**

19. Jina wanaloitana ndugu wa kike na wa kiume ni:
- **A) somo.**
- **B) umbu.**
- **C) mnuna.**
- **D) kaka.**

20. Chagua kundi la maneno ambayo ni Vihisishi.
- **A) Vile, lo, simile, mashallah**
- **B) Jamani, ingawa, Isipokuwa, huree**
- **C) Jamani, vyema, ila, inshalla**
- **D) Ala, ee, wee, lo**

21. Ni nini Udogo wa: Jito lile lina samaki wengi.
- **A) Kijito kile kina samaki wengi.**
- **B) Kijijito kile kina samaki wengi.**

© Eneza Education Limited *Creative Commons*

C) Kijito kile kina visamaki vingi.
D) Mto ule una samaki wengi.

22. Sentensi ipi haikuandikwa sawa kisarufi?
A) Jana jioni nilirudi.
B) Kesho jioni nitaondoka.
C) Jana asubuhi nitaondoka.
D) Kesho asubuhi nitarudi.

23. Tegua kitendawili hiki: Baba akipiga mbizi huibuka na ndevu nyeupe.
A) Mwiko
B) Muwa
C) Kinu
D) Mbegu

24. Chagua kiashiria radidi cha neno huku.
A) kukuku
B) kuku huku
C) kuko huku
D) huku huku

25. Sentensi ipi ni istiara?
A) Alikula chakula chote fyu.
B) Yeye anaringa kama tausi.
C) Kijana huyu ni simba.
D) Tulikuwa na furaha na buraha.

26. Nomino hizi hupatikana katika ngeli ipi?
Wingu, wazo, umbo.
A) U-ZI
B) I-ZI
C) U-YA
D) LI-YA

27. Baraza ni la Wabunge; baraza pia ni:
A) Mahali pa kuzungumzia
B) Barabara iliyowazi
C) Mahali mbali na bahari
D) Kitu kisicho sawa na kingine.

28. Kundi lipi lina majina ya mashairi?
A) Tarbia, mizani
B) Takhimisa mizani
C) Mishororo, vina
D) Tarbia, Takhmisa

29. Neno lipi ni kisawe cha neno takia?
A) taka
B) sofa
C) foronya
D) mto

30. "Nitaenda kuogelea kesho tukiwa na rafiki yangu" Ayubu alisema.
Andika katika usemi wa taarifa.
A) Ayubu alisema ataenda kuogelea siku iliyofuata akiwa na rafiki yake.
B) Ayubu alisema angeenda kuogelea siku iliyofuata akiwa na rafiki yake.
C) Ayubu alisema angeenda kuogelea kesho akiwa na rafiki yake.
D) Ayubu alisema naenda kuogelea siku iliyofuatia na rafiki yake.

Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40

Mashairi ni mojawapo ya Sanaa Kubwa yenye maana iliyofichika. Mashairi ni tungo zenye lugha nzuri iliyojaa utamu wa matamshi. Lugha ya kishairi hutumia maneno haba. Maneno haya huhifadhi maana kamili kama ilivyokusudiwa na mshairi.

Zipo aina mbalimbali za mashairi kama vile tathlitha, utenzi, tarbia, takhmisa na kadhalika. Aina hizi pia hujulikana kama bahari za Ushairi. Kila shairi la Kiswahili kawaida hugawanyika katika vifungu vinavyojulikana kama beti. Wingi au uchache wa beti kwenye shairi hutegemea uzito wa mawazo yanayoelezwa na mshairi. Kwenye ubeti hupatikana mishororo inayofuata mizani maalum kullingana na aina ya shairi. Hata hivyo aina ya tarbia ambayo hutumiwa na washairi wengi zaidi ya talhlitha na takhmisa, huwa na mizani kumi na sita kwa kila mshororo.

Mshairi ni mtu aliye na kipawa cha utungaji wa mashairi. Ni mtu anayeijua lugha kwa mapana na marefu na ni bingwa wa wa sanaa hii. Msanii kama huyu, huitwa manju au malenga. Mara nyingi mshairi anapoeleza jambo hutumia lugha kwa njia ya kipekee. Wakati mwingine mshairi hufupisha ama kurefisha maneno akilenga mtiririko wa mizani na vina bila matatizo. Kwa hivyo si jambo la ajabu kwamba mshairi huikuza na kuitukuza lugha kwenye tungo. Vilevile washairi huonyesha uzalendo kwa kuisifu nchi na viongozi wao katika mashairi yao.

© Eneza Education Limited Creative Commons

31. Maana iliyofichika ni sawa na
- **A) Maana iliyofichika**
- **B) Maana iliyofichamana**
- **C) Maana iliyofichua**
- **D) Maana iliyofichwa**

32. Maneno haba ni
- **A. Maneno machache**
- **B. Maneno madogo**
- **C. Maneno ya maana kamili**
- **D. Maneno ya habari kamili**

33. Ni sentensi ipi ambayo si sahihi kuhusu ushairi
- **A) Mashairi ni tungo zenye utamu wa matamshi**
- **B) Mashairi ni tungo zenye utamu wa mtiririko**
- **C) Mashairi ni tungo zenye utamu wa malenga**
- **D) Mashairi ni tungo zenye utamu wa maneno.**

34. <u>Bahari za ushairi wa</u> Kiswahili ni
- **A) Aina za takhmisa zinazojulikana**
- **B) Tathlitha utenzi na mishororo**
- **C) Mashairi yanayojulikana kama bahari**
- **D) Aina tofauti za mashairi**

35. Shairi la Kiswahili hugawanyika
- **A) Katika wingi na uchache**
- **B) Katika vina kadhaa**
- **C) Katika vifungu ama beti**
- **D) Katika beti rahisi**

36. Mishororo yenye mizani kumi na sita hupatikana kwenye?
- **A) tarbia**
- **B) tathlitha**
- **C) takhmisa**
- **D) Utanzi**

37. Neno lingine lililo na maana sawa na kipawa ni
- **A) kisanaa**
- **B) kipaji**
- **C) kipekee**
- **D) Kishairi**

38. Chagua jibu lililo sahihi zaidi
Mshairi huitwa bingwa kwa sababu:
- **A) anajua lugha anayoitumia**
- **B) yeye hufupisha na kurefusha maneno mengi matamu**
- **C) yeye ni mtungaji wa mashairi**
- **D) Ana ujuzi wa kipawa cha utungaji wa mahairi**

39. Kulingana na taarifa hii mshairi huonyesha uzalendo wake kwa
- **A) Kusifu nchi na viongozi wake**
- **B) Kutunga mashairi katika lugha nzuri**
- **C) Kuonyesha ubingwa wake wa lugha**
- **D) kufupisha maneno akilenga mizani**

40. Kichwa kinachofaa zaidi kwa habari hii ni:
- **A) Mshairi mwenye utamu wa matamshi**
- **B) Mshairi ni mtu mwenye kipawa**
- **C) Mshairi na aina za mashairi**
- **D) Mshairi na tungo za uzalendo**

<u>Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31-40.</u>

Nilikuwa nimelazwa hospitalini nilipopokea arafa kupitia rununu yangu. Ujumbe wenyewe ulikuwa wa kuatua na kuzusha moyo, ungechangia sana kuzorota kwa siha yangu lakini muuguzi wangu alisaidia kwa ushauri. Hiyo ilikuwa wiki ya sita tangu nilazwe pale kutokana na majeraha mikononi mwa majambazi katika barabara kuu.

Kwa mujibu wa hau wangu kijijini chote kilikuwa kimeinama. Wakaazi kumi na wanne walikuwa wameenda jongomeo kutokana na ulevi wa kileo haramu. Zaidi ya wahasiriwa ishirini nao walikuwa wakipigania uhai wao hospitalini. Walikuwa hali mahututi. Kati ya walioenda kuzimuni alikuwa msena wangu wa kufa na kuzikana.

Pindi nilipozipata habari zile, nilihuzunika kisha nikapandwa na mori. Nilishindwa nifanye yapi? Maswali tumbi nzima yaligongana akilini mwangu. Je, ni nani wa kulaumiwa kutokana na janga na jangamizi lile? Ni mgemaji au ni mlevi mwenyewe? Swali hilo lilinilemea kulijibu badala yake maswali mengine jakazidi ubongoni mwangu.

© Eneza Education Limited *Creative Commons*

Ni kwa nini binadamu razini akate shauri kutengenezea binadamu mwenziwe sumu ili tu ajipatie pesa? Je i wapi raha ya kujitajirisha kwa kuwaangamiza wenzake? Nusura ni muhukumu mgemaji akilini mwangu lakini ghafla swali jingine likazuka. Je, walevi hao nao, mbona wakakata shauri kuhatarisha maisha yao? Kwa nini wakakitumia kileo kile haramu? Hilo lilitokana na ukata, upuzaji, ukosefu wa matumaini maishani au nini?

Lakini umaskini upi? Nilijipata bado nikijisaili. Iwapo mtu amejipata maskini wa mali, lazima akubali kuwa maskini wa akili?

Serikali nayo je? Imefanya yote kuziangamiza pombe zile haramu? Mbona watu wachache wakubaliwe kujitajirisha kwa kuhatarisha maisha ya wenzao? Mbona wasichukuliwe hatua kali ili wawe funzo kwa wengine? Je, ni kweli vyombo vya usalama vimeshindwa kuuhiliki unyama huu au vinauvalia miwani? Ukweli ni kuwa serikali inao mkono mrefu. Inao uwezo wa kuondolea mbali uhalifu huo. Aidha raia wapenda wema lazima nao wachangie. Watoe habari kwa askari na watawala wahusika.

Nao maafisa ambao ni ndumakuwili sharti wachukuliwe hatua. Ni bayana kuwa, baadhi ya maafisa katika vyombo vya usalama si waadilifu. Wao hushirikiana na wagemaji wale wenye ubinafsi. Hao ndio wanaoharibia jina vyombo vya usalama kwani nazi moja ikioza harabu ya nzima.

41. Mwandishi alilazwa hospitalini kwa nini?
- **A) Kulewa pombe haramu**
- **B) Kupata ajali ya barabara**
- **C) Kushtuka moyo**
- **D) Kuvamiwa na wakora**

42. Mwandishi alipataje habari za janga Kijijini?
- **A) Kupitia kwa ujumbe mfupi kwa simu.**
- **B) Kupitia kwa muuguzi.**
- **C) Kupitia rediono**
- **D) Kupitia kwa wagonjwa wenzake**

43. Yaelekea ni watu wangapi walionusurika janga lile?
- **A) Hatujaambiwa**
- **B) Kumi na wanne**
- **C) Takribani ishirini**
- **D) Thelathini na wanne**

44. Kwa maoni ya mzungumuzaji nani anayestahili lawama?
- **A) Mgemaji wa tembo haramu**
- **B) Mlevi wa tembo haramu**
- **C) Vyombo vya usalama**
- **D) Jamii kwa jumla**

45. Yapi huelekeza watu kujihusisha na unywaji wa tembo haramu?
- **I. Ukosefu wa pesa**
- **II. Kiu**
- **III. Upuuzaji**
- **IV. Ukosefu wa elimu**

A i, ii, iii
B. i, iii, iv
C. ii, iii, iv
D. i, ii, iv

46. Ni sahihi kusema
- **A) Mwandishi ni mlevi aidha**
- **B) Mwandishi ni mfisadi**
- **C) Mwandishi ni mwadilifu**
- **D) Mwandishi ni mnafiki**

47. Nini maana ya <u>Maafisa ambao ni ndumakuwili.</u>
- **A) Wapendao maendeleo**
- **B) Wapokeao hongo**
- **C) Hawana ubinafsi**
- **D) Wanaojali kazi zao**

48. Ipi ni methali
- **A) Kwenda jongomeo**
- **B) Pandwa na mori**
- **C) Nazi moja ikioza harabu ya nzima.**
- **D) Maafisa ambao ni ndumakuwili.**

49. Kwa nini wauza pombe huendelea na biashara yao haramu?
- **A) Kuna ufisadi kwa baadhi ya viongozi**
- **B) Hawajulikani na askari**
- **C) Serikali inawahurumia**
- **D) Serikali haina uwezo wa Kuwakamata.**

50. Kichwa Kipi kinafaa zaidi kwa habari hii?
- **A) ulevi wa pombe**
- **B) Serikali na pombe haramu**
- **C) Ugemaji wa pombe haramu**
- **D) Wanakijiji kumi na wanne kwenda jongomea.**

© Eneza Education Limited *Creative Commons*

© Eneza Education Limited
Creative Commons